


# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Telegramu: "CABINET" DAR ES SALAAM  
Simu: 2116898, 2116900/6  
Barua pepe: chief@ikulu.go.tz  
Barua pepe: ikulu@ikulu.go.tz  
Nakushi: 2113425/2116914/2117272  
Unapojibu tafadhali taja:



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA BARACK OBAMA,  
11400 DAR ES SALAAM.

Kumb. Na. SAB. 228/732/01/B/141

30 Mei, 2014

**Yah: MWALIKO WA KUHUDHURIA WARSHA YA KUPATA MAONI YA  
WADAU KUHUSU MPANGO KAZI WA MPANGO WA KUENDESHA  
SHUGHULI ZA SERIKALI KWA UWAZI (OGP) WA AWAMU YA PILI**

Tafadhali husika na somo hilo hapo juu.

Kama mnavyofahamu, Tanzania ni mwanachama wa Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (*Open Government Partnership – OGP*) tangu mwezi Septemba, 2011. Mpango Kazi wa utekelezaji wa mwaka mmoja uliandaliwa kwa kushirikisha Asasi za Kiraia na kuanza utekelezaji.

Hivi sasa, tuko katika mchakato wa kuandaa Mpango Kazi wa miaka miwili kuanzia mwaka 2014/15. Uandaaji wa Mpango Kazi huo hauna budi kushirikisha wadau mbalimbali kutoka sekta ya umma na binafsi.

Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha katika warsha ya siku moja ya kupata maoni ya wadau kuhusu Mpango Kazi wa OGP Awamu ya Pili utakaotekelezwa katika kipindi cha 2014/15 – 2015/16.

Mwaliko huu unazingatia dhana ya ushirikishwaji unaotumika katika Utekelezaji wa Mpango wa OGP ambao Sekta ya Umma na Asasi zisizo za Kiserikali kuandaa na kutekeleza Mpango kazi kwa pamoja.

Warsha iliyopangwa tarehe 29 Mei, 2014 haikufanyika kutokana na sababu zilizokuwa nje ya uwezo wetu. Warsha hiyo sasa itafanyika tarehe 09 Juni, 2014 katika ukumbi wa Makumbusho ya Taifa uliopo karibu na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kuanzia saa 2:30 asubuhi. Ratiba imeambatanishwa.

Tafadhali thibitisha ushiriki wako kwa kuwasiliana na Bw. Mathias Chitunchi kwa simu Na. 0754 856 452 barua pepe [mchitunchi@hotmail.com](mailto:mchitunchi@hotmail.com), au Bw Evarist Kamwaga kwa simu Na. 0717 144 828 barua pepe [ekamwaga@twaweza.org](mailto:ekamwaga@twaweza.org).

Tunatarajia ushiriki wako au tuma mwakilishi.

  
S. Mlawi

Kny: KATIBU MKUU KIONGOZI